

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA AKABIDHI KADI 220 ZA BIMA YA AFYA KWA WATOTO YATIMA NA WAISHIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo amekabidhi kadi 220 za Bima ya Afya (Toto Afya Card) zenye thamani ya zaidi ya shilingi Million 11 kwa watoto yatima na waishio Kwenye mazingira magumu ili wapate uhakika wa matibabu mwaka mzima ikiwa ni sehemu ya Mwezi mtukufu wa Ramadhan.

RC Makonda amesema kwa kawaida Mwezi wa Ramadhan watu wamekuwa wakifuturisha watoto yatima lakini inakuwa ni chakula cha siku moja kwaiyo katika mwendelezo wa mwezi mtukufu ameona ni vyema aguse maisha ya watoto yatima kwa kuwapatia uhakika wa matibabu kwa kuwapatia Bima ya Afya ambapo ameamua kuanza na watoto 220 na baadae ataongeza wengine.

Aidha RC Makonda amesema kadi hizo zitawawezesha watoto kupatiwa matibabu Bure kwa kipindi cha mwaka mmoja katika Hospitali yoyote hapa nchini.

Hata hivyo RC Makonda amesema watoto waliopatiwa kadi hizo hawahusiani na wale waliojitokeza kwenye Zoezi la kutafuta haki ya mtoto ambapo ameshukuru Hospital ya Regency na TMJ kwa kujitolea kutoa kadi hizo.

Sambamba na hilo RC Makonda amesema atakabidhi pia mabegi 400 yaliyosheheni vifaa vyote vya Shule kwa vituo vya watoto yatima na waishio kwenye mazingira magumu ili wawe na uhakika wa kupata masomo mwaka mzima na kuweza kutumia vyema fursa ya elimu bure.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Hospital ya Regency Dr. Kanabar Rajni na Mkurugenzi wa hospital ya TMJ Bi. Parul Chhaya kwa pamoja wamesema wameguswa kutoa msaada huo Kama sehemu ya kuunga mkono hamasa anayoitoa RC Makonda kwa wazazi kuwa na kadi za bima za afya (Toto Afya Card).

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

13/06/2018